



UNIVERSITY OF CAMBRIDGE INTERNATIONAL EXAMINATIONS
General Certificate of Education Ordinary Level

SWAHILI

Paper 1

3162/01

May/June 2009

3 hours

Additional Materials: Answer Booklet/Paper

READ THESE INSTRUCTIONS FIRST

If you have been given an Answer Booklet, follow the instructions on the front cover of the Booklet.

Write your Centre number, candidate number and name on all the work you hand in.

Write in dark blue or black pen.

Do not use staples, paper clips, highlighters, glue or correction fluid.

Answer **all** questions.

At the end of the examination, fasten all your work securely together.

The number of marks is given in brackets [] at the end of each question or part question.



This document consists of **6** printed pages and **2** blank pages.



Section A – Translation**1** Translate the following passage into **English**:

Roda asingeweza kufanya jambo lo lote la kuiepusha ajali ile. Alikuwa katika gari na mtoto wake aitwaye George mwenye umri wa miaka minne. Alikuwa anampeleka George kwenda kushinda nyumbani kwa mama yake Roda, yaani bibi yake George. Roda alikuwa amesimamisha gari kwenye taa zinazoongoza magari barabarani, akingoja ishara ya taa kijani ili aendelee na safari yake. George alikuwa kwenye kiti cha nyuma.

Mara, kwa ghafula, akaiona gari ikiwajia kutoka kushoto. Dereva wa gari hiyo alishindwa kuizungusha kabisa alipokuwa anakata kona, ikagongana na gari ya Roda kwa kishindo kikubwa. Roda alisukumwa mbele, lakini kwa bahati nzuri ukanda ukamzuia. Pia puto (bofu) la mpira likachipuka kutoka kwenye usukani likavimba kwa hewa. Hivyo likamzuia Roda kugongwa na usukani. Akanusurika.

Moyo ulimdunda. Akamfikiria mtoto wake. “George!” akapiga ukelele. “Mwanangu, mzima?” akauliza Roda kwa sauti ya kutetemeka. “Ndio, mama” George akajibu pole pole. Ingawa ajali ilimshitua George, hakuumia kwa vile ukanda aliomvika mama yake ulimnusuru naye pia. Roda alitokwa na machozi kuisikia sauti ya mtoto wake. [20]

2 Translate the following passage into **Swahili**:

When my brother-in-law, John, first mentioned to me that he wanted to climb Mount Kilimanjaro, I thought he was joking. That was in November last year. After that, he and his wife (my sister) Agnes talked about it constantly to me and to their friends. They also started preparing themselves for the climb by performing different exercises every day. They also went for long walks in the morning and in the evening.

They climbed Mount Kilimanjaro two months ago. The task was not easy, but they enjoyed the experience. Agnes and John said that they received much help from their colleagues. Climbers encouraged and helped one another in overcoming the problems they faced along the way. I asked John what baggage did he take with him on their route. He said that, apart from food, the most important items were clothes and equipment.

John and Agnes are proud of their achievement. They are also proud of the fact that Mount Kilimanjaro is in East Africa! It is a beautiful mountain. It attracts hundreds of tourists every year to Tanzania and Kenya. Not all come to climb it; many are happy simply to view it. [30]

Section B – Comprehension

3 Read the text and answer the questions that follow in **Swahili**:

Simu za mkononi Ziwa Viktoria

Jina langu ni Mariamu, nami ni mwandishi wa habari. Hivi karibuni nilipanda boti Ziwa Viktoria kwa kazi fulani. Nilistaajabu kuona kwamba simu yangu ya mkononi ilipokea ujumbe ingawa nilikuwa mbali sana na nchi kavu!

Mtu aliyekuwa amekaa ubavuni mwangu kwenye boti pengine alihisi nilivyoshangaa. Alijijulisha, akasema jina lake ni Solomon Mukazi; ana cheo cha juu katika mojawapo za kampuni za simu zinazohudumia eneo lile. Kampuni yake na baadhi ya kampuni nyingine zinashirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki na vikundi visivyo vya serikali katika mradi mkuu wenye lengo la kuboresha mawasiliano ya simu za mikononi kwenye ziwa hilo. Alinieleza kwamba kampuni za simu zimechunguza kwa muda wa miaka miwili namna ya kutoa huduma bora kwa watu wapatao milioni 30 wa Tanzania, Kenya na Uganda wanaoishi kando ya ziwa. Kampuni za simu zinajenga pia vituo vya mawasiliano ili kuongeza usikivu wa simu kwa umbali wa kilomita 20 ziwani. Ujenzi wa vituo utakapomalizika mnamo miezi sita kutoka sasa, watu wataweza kupiga na kupokea simu na kupeleka na kupokea ujumbe kutoka aghalabu pande zote za ziwa.

Ingawa aliyonieleza Bwana Mukazi yalikuwa mambo ya kuvutia, bado sikufahamu kwa nini serikali ikafikiri mradi huu ni muhimu mno. Kwani watu wangezungumza mambo muhimu gani katikati ya ziwa? Bwana Mukazi akajibu kwamba mradi ulianzishwa kwa madhumuni hasa ya kuwasaidia takriban wavuvi 200,000 wa Ziwa Viktoria kwa vile wanahitaji sana njia thabiti za mawasiliano pale wanapokabili hali ya hatari au dharura. Nilishtuka kusikia kwamba idadi kubwa ya watu hupoteza maisha yao hapo ziwani ama kwa kupatwa ajali, au kwa vitendo vya wizi na maharamia. Akaendelea: “Ni wazi kwamba mradi huu ni muhimu. Hivyo inabidi tufanye kazi upesi ili tuliondoshe tatizo hili.”

Nikamwambia sasa nahisi nimo katika hali ya usalama kama msafiri, nikijua kwamba ninaweza kupata msaada ikiwa itatokea hali ya hatari. Akaendelea: “Pia usisahau kama hata baada ya hali hiyo kutokea, unaweza kuwasiliana upesi na jamaa na marafiki wakupendao ili kuwatuliza moyo kuhusu hali yako. Miezi michache tu iliyopita, watu waliopatwa na ajali kwenye boti moja waliweza kuwasiliana na familia na marafiki zao upesi tu baada ya ajali kuwaambia kwamba wao hawajambo. Wasingeweza kufanya hivyo miaka miwili iliyopita.

Niliposhuka Kisumu kutoka kwenye boti, nilizungumza na mvuvi wa hapo. Nikamueleza aliyoniambia Bwana Mukazi. Si atakubaliana na Bwana Mukazi kwamba vitegauchumi vilivyotumiwa kuikuza teknolojia ya kampuni za simu vimeleta faida kubwa kwa jamii ya wavuvi wa Ziwa Viktoria? Alisita kabla ya kulijibu swali langu huku akiinua mabega. Akasema: “Nafurahi teknolojia inatuletea njia za usalama, lakini naona kuna mambo mengi mengine yanayohitaji pia kushughulikiwa. Kiwango cha maji ziwani kinashuka. Pia kuna uharibifu wa mazingira. Matatizo haya ya kimazingira yanaathiri ubora wa maji ya ziwa ambayo tena hudhuru ndege na – muhimu kwetu sisi – hudhuru samaki.” Alipendekeza kwamba badala ya kutumia pesa zote kuboresha teknolojia ya simu za mkononi itakuwa bora zaidi ikiwa baadhi ya pesa hizo zitatumiawa kuboresha hali ya ziwa kwa jumla.

* * *

Jibu maswali yafuatayo kwa Kiswahili ukitumia maneno yako mwenyewe kadiri iwezekanavyo. Andika sentensi nzima. Usijibu kwa kukariri tu au kunukuu maandishi yalivyoandikwa kwenye kifungu hapo juu.

Now answer the questions in your own words, as far as possible. You should avoid copying word-for-word from the text.

- (a) Kwa nini Mariamu alikwenda Ziwa Viktoria? [1]
- (b) Mariamu alifanyaje alipoona kwamba simu yake ya mkononi inapokea ujumbe, na kwa nini akaathirika hivyo? [2]
- (c) Kwa nini Bwana Mukazi akaanza kuzungumza na Mariamu? [1]
- (d) Mbona Bwana Mukazi anajua habari hizi za simu za mikononi katika eneo hili? [1]
- (e) Tunajuaje kutokana na kifungu hiki kwamba mradi huu wa simu za mikononi ni mradi wa kimataifa? [1]
- (f) Kutokana na kifungu hiki tunapata kujua sababu gani ya ujenzi wa vituo vya mawasiliano? Lini watu watarajie kupata huduma bora? [2]
- (g) Kikundi gani kinakusudiwa hasa kufaidika na mradi huu? Mradi utawasaidia vipi? [2]
- (h) Kwa nini Bwana Mukazi anafikiri mradi huu utekelezwe kwa haraka? [1]
- (i) Kwa nini Bwana Mukazi akamueleza Mariamu habari ya ajali ya boti? [1]
- (j) Kwa nini mvuvi akasita kabla ya kulijibu swali la Mariamu? [1]
- (k) Ni nini mawazo ya mvuvi kuhusu mradi wa simu za mikononi, na mawazo haya yanatofautiana vipi na yale ya Bwana Mukazi? [4]
- (l) Baada ya kusoma kifungu hapo juu, andika kifungu kidogo cha maneno 20 hivi ukitoa maoni yako kuhusu mradi wa simu za mkononi. [1]
- (m) Eleza maana ya:
- (i) “nilikuwa mbali sana na nchi kavu”, na [1]
- (ii) “kiwango cha maji ziwani kinashuka”. [1]

[20 for Content + 5 for Language = 25]

Section C – Composition

- 4 Write a composition of about **120** words in **Swahili** on **one** of the following subjects.
- (a) Describe the celebration of an event in the family.
 - (b) 'You must have money in order to succeed in life and to be happy.' Discuss.
 - (c) Write a letter to a newspaper suggesting ways of reducing pollution in the world.

[25]

Permission to reproduce items where third-party owned material protected by copyright is included has been sought and cleared where possible. Every reasonable effort has been made by the publisher (UCLES) to trace copyright holders, but if any items requiring clearance have unwittingly been included, the publisher will be pleased to make amends at the earliest possible opportunity.

University of Cambridge International Examinations is part of the Cambridge Assessment Group. Cambridge Assessment is the brand name of University of Cambridge Local Examinations Syndicate (UCLES), which is itself a department of the University of Cambridge.